HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

HOTUBA YA MSTAHIKI MEYA WA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI MH. BENJAMINI KAWE SITTA, KUHUSU MAKISIO YA BAJETI YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI KWA KIPINDI CHA JULAI 2017 – JUNI 2018, ILIYOSOMWA KWENYE MKUTANO MAALUM WA BARAZA LA MADIWANI TAREHE 08/MACHI/2017

IMETAYARISHWA NA:

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI,
S.L.P. 31902,
2 BARABARA YA MOROGORO
14883 DAR ES SALAAM
SIMU: 022 2170173
FAX: 022 2172606
Tovuti: www.kinondonimc.go.tz

MACHI, 2017

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni.
Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni,
Ndugu Katibu Tawala wa Wilaya ya Kinondoni na
Makatibu Tarafa kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni,
Ndugu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na Watendaji, Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana.

Naomba kuanza Hotuba yangu kwa kumshukuru mwenyezi Mungu, kwa kuniruhusu kusimama mbele yenu kuwasilisha Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa Mwaka wa fedha 2017/2018.

Waheshimiwa Madiwani na wajumbe waalikwa; napenda kutumia fursa hii hadhimu kuwapongeza kwa dhati Waheshimiwa Wabunge na Madiwani kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kuweza kuongoza Majimbo na Kata zenu kwa kipindi cha miaka mitano (2015-2020),Hongereni sana.Lakini pia Waheshimiwa Madiwani na wajumbe waalikwa kama mnavyojua kwamba Halmashauri yetu ya Kinondoni sasa imegawanyika na kuweza kuwa na Halmashauri mpya ya Ubungo nachukua nafasi hii kwanza kwa kujipongeza mimi mwenyewe kwa kuchaguliwa kuwa Meya wa Manispaa ya Kinondoni,vilevile nimpongeze Mheshimiwa Mangaru Manyama Diwani wa Kigogo kwa kuchaguliwa kwake kuwa Naibu Meya bila kuwasahau waheshimiwa Madiwani wote walichaguliwa kuwa wajumbe na wenyeviti wa Kamati za kudumu za Halmashauri, Hongereni sana.

Wahesimiwa Madiwani na wajumbe waalikwa; Kabla ya kuwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2017/2018, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine kutayarisha bajeti hii ambayo maandalizi yake yamehusisha wadau wengi. Napenda kuwashukuru wananchi kwa pamoja kwa kuibua miradi katika ngazi ya Mitaa na Kata inayolenga kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii ambayo ndiyo tumeyafanyia kazi katika kundaa mpango na bajeti hii.

Nachukua fursa hii pia kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uongozi, Kamati ya Huduma za Uchumi, Afya na Elimu na Wajumbe wa Kamati ya Mipango Miji na Mazingira, Baraza la Wafanyakazi, Kikao cha Ushauri cha Wilaya (DCC) na Kamati ya Kudhibiti UKIMWI ya Manispaa kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuchambua na kutoa ushauri katika kuandaa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2017/2018. Ushauri wa wajumbe wa kamati hizo pamoja na ushauri wa Sekretarieti ya Mkoa umesaidia sana kuboresha mpango na bajeti ninayoiwasilisha leo.

Waheshimiwa Madiwani na wajumbe waalikwa; hotuba yangu itajikita katika mambo makuu matatu ambayo ni, kwanza, ni mwelekeo wa Halmashauri yetu katika kujenga misingi ya uchumi imara, pili mapitio ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa fedha 2016/2017 na tatu, malengo ya fedha kwa Mwaka 2017/2018.

MWELEKEO KATIKA KUJENGA MSINGI WA UCHUMI IMARA.

Waheshimiwa Madiwani na wajumbe waalikwa; azma ya Serikali ya awamu ya tano ni kuifikisha Tanzania kuwa nchi yenye kipato cha kati ifikapo Mwaka 20125. Ili kufikia azma hii, ni muhimu kuwekeza katika viwanda kama ilivyosisitizwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt John Pombe Joseph Magufuli akizindua Bunge la 11 tarehe 20 Novemba 2015.

Waheshimiwa Madiwani na wajumbe waalikwa; Sisi kama Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni tumejipanga kuchukua hatua madhubuti zinazolenga kuijenga Halmashauri yetu kwa kukuza uchumi na kupunguza umasikini kwa wananchi wetu. Moja ya hatua hizo ni kusimamia na kufuatilia kwa ukamilifu Utekelezaji wa Mpango wa pili wa Maendeleo wa miaka mitano 2016/2017 – 2020/2021, mpango ambao umejikita katika kujenga msingi wa uchumi wa viwanda na maedeleo ya watu.

Waheshimiwa Madiwani na wajumbe waalikwa; Ili mpango huu uwezekutekelezeka kwa ufanisi na kupata matokeo tarajiwa, ni dhaihiri kuwa tutahitaji rasilimali za kutosha,hususani rasilimali fedha. Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa kushirikiana na wadau wengine inalo jukumkumu la kuimrisha ukusanyaji wa mapato ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha.Aidha Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020 imeweka bayana majukumu ya Serikali za Mitaa ya kuimarisha usimamizi na ukusanyaji wa mapato, kupanua wigo wa vyanzo vipya vya

mapato na kusimamia kwa ufanisi matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali.

Waheshimiwa Madiwani na wajumbe waalikwa; Kwa upande wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato, Halmasahuri yetu itajielekeza katika maeneo yafuatayo;- Kusimamia kikamilifu matumizi ya Vifaa na mifumo ya Kielectroniki katika uksanyaji wa mapato ya Halmashauri ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato.Kuimarisha ufuatiliaji wa mapato yanayokusanywa na wazabuni/Taasisi (TRA) mbalimbali ili kuongeza mapato yetu.

Waheshimiwa Madiwani na wajumbe waalikwa; Halmashauri itazingatia sheria, kanuni, taratibu, miongozo na kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kuthibiti matumizi ya fedha za umma. Hii ni pamoja na kuthibiti matumizi yasiyo ya lazima kama safari za nje, sherehe, warsha na semina.Aidha, Halmashauri itaimirisha mfumo wa manunuzi ili kupata vifaa na Miradi yenye ubora wenye thamani halisi.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2016/2017

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa; Ili kuweza kutekeleza malengo yaliyopangwa, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeweka vipaumbele katika maeneo yafuatayo: -

I. Kuboresha na kuimarisha ukusanyaji wa Mapato ya Manispaa kwa kuziba mianya ya uvujaji wa mapato na kubuni vyanzo vipya vya mapato.
II. Kuboresha miundombinu ya Afya, Shule za Msingi na Sekondari.
III. Kuboresha upatikanaji wa huduma za mama na mtoto ili kupunguza vifo vya mama na mtoto.

IV. Kuboresha miundombinu ya maji, umeme, barabara, mifereji ya maji ya mvua na Kilimo mjini.
V. Kuboresha hifadhi ya mazingira na uzoaji na wa taka ngumu na maji taka.
VI. Kuimarisha ushirikishwaji wa jamii katika upangaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
VII. Kuboresha mazingira ya wafanyabiashara ndogondogo kwa kutenga fedha kwa ajili kujenga masoko ya Manispaa na mabanda ya wafanya biashara ndogondogo.
VIII. Kuinua kipato cha wanawake na vijana kwa kuendelea na utaratibu wa kuwapatia elimu ya ujasiriamali na mikopo yenye masharti nafuu.

MAPATO YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa; Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa Mwaka wa fedha 2016/2017 **baada ya mgawanyo wa Bajeti ya Ubungo na Kinondoni,** Manispaa ya Kinondoni inatarajia kukusanya fedha kiasi cha **Tsh. 154,248,195,864.00.** Kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na Ruzuku ya Serikali **Tsh.107,805,094,178.00, Tsh.37,684,857,819.00** makusanyo ya ndani ya Halmashauri,**Tsh.710,000,000.00** ni mchango wa nguvu za wananchi na **Tsh. 8,048,243,867.00** fedha za mfuko wa Barabara (Road Fund)).

MATUMIZI YA KAWAIDA MWAKA 2016/2017.

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa;Katika Mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri iliidhinisha matumizi ya kawaida ya **Tsh.62,054,205,798.00** kati ya fedha hizi **Tsh.51,482,595,704.00** ni fedha za Ruzuku ya Serikali zikijumuhisha **Tsh.48,663,241,400.00** kwa ajili ya

Mishahara(PE) na **Tsh.2.819,354,304.00** matumizi ya kawaida(OC).**Tsh.10,571,610,094.00** ni fedha za Halmashauri, **Tsh.1,027,080,000.00** kwa jili ya Mishahara(PE) na **Tsh.9,544,530,094.00** Matumizi ya kawaida.

MATUMIZI YA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2016/2017.

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa;kwa upande wa matumizi ya Miradi ya Maendeleo,Jumla ya **Ths.92,195,990,066.00** ziliidhinishwa, kati ya fedha hizo **Tsh.56,324,498,474.00** ikiwa ni fedha za Ruzuku ya Serikali,**Tsh.35,871,491,592.00.00** ni fedha za Manispaa zikijumuhisha fedha za uchangiaji huduma(Cost sharing) na Mchango wa nguvu za wananchi.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2016/2017

Waheshimiwa Madiwani na wajumbe waalikwa; Kabla ya kuwasilisha bajeti ya mwaka 2017/2018 ni vyema tukapata fursa ya kujua mafanikio na changamoto ambazo tumekutana nazo katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2016/2017. Tathmini inaonyesha kuwa katika kutekeleza bajeti ya mwaka 2016/2017 Halmashauri imetoa huduma kwa wananchi wake kwa ufanisi katika maeneo ya Usafi wa mazingira, Elimu ya Msingi na Sekondari, Utoaji wa huduma za Afya, Miundombinu ya barabara na Maji, Uwajibikaji na Utawala Bora. Aidha Halmashauri imeendelea kuimarisha upatikanaji wa nyenzo za kufanyia kazi kwa watumishi wake hadi ngazi ya Kata hali iliyoimarisha usimamizi wa kazi katika maeneo ya miradi na utoaji wa huduma zingine kwa jamii.

UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017.

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa; Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ilipanga matumizi ya makadirio ya makusanyo hayo kama ifuatavyo; Fedha kutoka Serikali Kuu kiasi cha **Sh. 107,805,094,178.00** zilipangwa kutumika kama ifuatavyo; **Sh.48,663,241,400.00** ni kwa ajili ya mishahara, **Sh.2,819,354,304.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Sh. 56,322,498,474.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Fedha za makusanyo ya ndani (own source) **Sh. 37,684,857,819.00** zilipangwa kutumika kama ifuatavyo; kiasi cha **Sh. 27,113,247,725.00** zilipangwa kutekeleza miradi ya maendeleo, **Sh. 1,027,080,000.00** mishahara na **Sh.9,544,530,094.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha **Sh.8,048,243,867.00** zinazotolewa na TAMISEMI zilipangwa kutekeleza miradi ya Barabara.

HALI YA UKUSANYAJI WA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI HADI DISEMBA, 2016

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa; Ukusanyaji wa Mapato kwa mwaka **2016/2017 kabla ya mgawanyo wa Bajeti ya Manispaa ya Ubungo na Kinondoni** hadi kufikia mwezi Disemba, 2016 Halmashauri imekusanya jumla **Sh.69,344,072,230.23** sawa na asilimia **28.56** ya bajeti **Tsh.242,812,087,810.00**. Kati ya fedha zilizokusanywa kiasi cha **Sh.20,666,882,569.28** sawa na asilimia **32.1** ya lengo la makusanyo ya ndani ya **Sh.64,285,690,000.00.** Aidha, fedha kiasi cha **Sh.42,284,723,988.00** ni mapokezi ya fedha za ruzuku za matumizi ya kawaida sawa na asilimia **41** ya lengo la **Sh. 103,043,853,800.00.** Kiasi cha **Sh.204,345,846.00** ni michango ya nguvu za wananchi sawa na asilimia **14.4** ya lengo la **Sh.**

1,420,000,000.00 na pia Halmashauri imepokea kiasi cha **Sh.6,188,119,826.00** ikiwa ni ruzuku za miradi ya maendeleo sawa na silimia **0.08** a lengo la kupokea **Sh. 74,062,544,009.97.00** kwa mwaka. Jedwali Na. 1 Ukurasa wa 9 linafafanua.

JEDWALI 1: MAKADIRIO YA MAPATO YA BAJETI 2016/17 YAKILINGANISHWA NA MAKUSANYO HALISI HADI DISEMBA, 2016

CHANZO	MAKISIO YA BAJETI 2016-17	MAKUSANYO JULAI 2016 HADI DISEMBA 2016	%
MAPATO	**1**	**2**	**(2/1)**
MAPATO YA NDANI	**64,285,690,000.00**	**20,666,882,569.28**	32.1
RUZUKU YA SERIKALI			
MISHAHARA (PE)	97,326,482,800.00	40,366,821,176.02	41.4
MATUMIZI YA KAWAIDA	5,717,371,000.00	1,917,902,812.00	33.5
JUMLA NDOGO: PE NA OC	**103,043,853,800.00**	**42,284,723,988.02**	41.0
RUZUKU YA SERIKALI – MIRADI YA			
MAENDELEO			
HEALTH BUSKET FUNDS	3,531,019,000.00	1,765,509,500	50.0
LGDG (CBG+CDG)	6,388,616,000.00	1,118,548,000.00	17.5
RWSSP-(CDG & CBG)	155,280,000.00	69,751,240.65	44.9
LDF	10,415,000.00	0	0
ROAD FUND – MAINTENANCE	12,281,790,009.97	3,008,131,086.28	24
CONTITUENTS FUND	176,522,000.00	226,180,000.00	128.1
SEDP	242,680,000.00	0	0
PRIMARY SPECIAL SCHOOL	150,000,000.00	0	
DMDP	51,126,222,000.00	0	0
JUMLA NDOGO:	**74,062,544,009.97**	**6,188,119,826.93**	
MICHANGO YA WANANCHI	1,420,000,000.00	204,345,846.00	14.4
JUMLA YA BAJETI	**242,812,087,810.00**	69,344,072,230.23	28.56

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa; Sina budi kuwashukuru wachangiaji wote katika bajeti yetu ya mwaka 2016/2017, wakishirikiana na wananchi wote wa Kinondoni kwa michango yao ambayo kwa pamoja imetuwezesha kutoa huduma kwa wananchi na kutekeleza miradi mbalimbali katika mwaka huu wa fedha utakaoishia Juni 2017.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2016/2017

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa; Kwa mwaka 2016/2017 Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni baada ya mgawanyo wa Halmashauri ya ubungo, Kinondonii ilikadiria kutumia

Sh. 92,193,990,066.00 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Sh.56,322,498,474.00** ni Ruzuku ya Serikali Kuu, **Sh. 8,048,243,867.00** ni mfuko wa barabara, **Sh.27,113,247,725.00** ni vyanzo vya ndani ikiwa ni pamoja na **Sh. 710,000,000.00** zinazotokana na Nguvu na michango ya wananchi.

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa; Hadi kufikia Disemba 31,2016 Halmashauri imetumia jumla ya **Sh. 56,960,629,433.56** sawa na asilimia **37** ya makisio ya bajeti baada ya mgawanyo. Kati ya fedha hizo **Sh. 13,413,545,214.99** fedha za mapato ya ndani ikijumuisha miradi **Sh. 7,287,811,192.99.00,** matumizi mengineyo **Sh**. **5,171,454,576.00 Sh. 749,933,600.00** ni mishahara na **Sh.204,345,846.00** michango ya nguvu a wananchi. Jumla ya fedha ya Ruzuku toka Serikali kuu zilizotumika ni **Sh 43,547,084,218.55** zikijumuisha Mishahara **Sh. 40,366,821,176.02** Matumizi mengineyo **1,917,902,812.00** na Miradi ya Maendeleo **Sh 1,262,360,230.55.**

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI VIPORO YA MWAKA YA 2015/2016 HADI DISEMBA, 2016

Fedha za Bakaa kwa miradi ya maendeleo ya mwaka 2015/2016 zilikuwa ni **Tsh. 6,535,938,929.84** kutoka vyanzo mbalimbali. Kati ya fedha hizo **Tsh**. **291,573,000.00** ni fedha za HIV/AIDS UKIMWI, **Tsh. 737,000,156.23** ni fedha za Basketi na **Tsh. 5,507,365,773.61** ni fedha za Mfuko wa Barabara. Matumizi ya fedha hizi hadi Disemba, 2016 ni **Tsh. 333,850,516.92**

MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

Katika kutekeleza miradi ya maendeleo ya Mwaka kwa kipindi cha kuanzia Julai hadi Disemba 2016 Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imefanikisha Miradi mbalimbali. Baadhi ya miradi hiyo ni kama ifuatayo:

SEKTA YA MAJI:

Mafanikio katika Sekta ya Maji

Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai hadi Disemba 2016, sekta ya Maji imeweza kupata mafanikio katika maeneo yafuatayo:

i) Kukamilisha kwa ujenzi wa mradi wa maji Makongo -Mbuyuni (RWSSP), Makongo Juu, Kigogo Mbuyuni na Msasani Makangira.

ii) Kutatua migogoro ya uendeshaji kamati za maji za Makongo Mbuyuni, Madale Kisauke, Tandale na Kinondoni mjini na Bwawani

iii) Utoaji wa elimu jinsi hifadhi ya mazingira na uendeshaji wa miradi ya Maji hususani ngazi ya Jamii.

CHANGAMOTO ZINAZOKABILI SEKTA YA MAJI:

Sekta ya maji katika Manispaa ya Kinondoni inakabiliwa na changamonto nyingi kama ifuatavyo:-

i) Uwezo mdogo wa vyanzo vya maji vilivyokwishabainishwa,

iii) Upotevu wa maji mengi katika mtandao wa mabomba ya kusafirisha na kusambaza maji,

iv) Watumiaji kutokulipia ankara za maji,

v) Gharama kubwa za miundombinu ya maji,

vi) Uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji,

vii) Uharibifu wa miundombinu,

MIKAKATI YA KUBORESHA HUDUMA YA MAJI KATIKA HALMASHAURI

i) Kuunda vyombo vya watumia maji ili wananchi waweze kusimamia na kuendesha miradi yao ya maji katika ngazi ya Jamii.

ii) Kushirikiana na Wadau mbalimbali ili kuweza kupata fedha na kutekeleza Miradi mikubwa ya maji ya kuihudumia jamii.

iii) Kutoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali juu ya hifadhi ya mazingira na uendeshaji wa miradi ya Maji hususani ngazi ya Jamii.

iv) Kushirikisha Sekta binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa huduma ya maji katika ngazi zote.

v) Kushirikiana na DAWASA katika utekelezaji wa mpango wa muda mrefu wa kuboresha vyanzo vya maji vilivyopo ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa vyanzo vipya vya maji

SEKTA YA ELIMU SEKONDARI:

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

Kwa kipindi cha mwaka 2016, Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imeweza kufanikisha mambo yafuatayo katika shule za sekondari:

1. Kuboresha hali ya miundombinu katika shule zote za Serikali **22** Kama vile kuongezeka Kwa idadi ya Vyumba vyama darasa, Vyoo, Maabara na madawati kwa shule za sekondari
2. Kuongezeka Kwa Idadi ya walimu kutoka walimu **786** mwaka **2015** hadi walimu **802** Mwaka 2016.
3. Kutoasemina elekezi Kwa wakuu wa shule zote **22** juu ya usimamizi na uendeshaji wa shule na usimamizi wake kwania ya kuongeza ufanisi katika utendajikazi wake.
4. Kuongeza idadi ya shule zilizokuwepo mwaka **2015** toka **22** hadi kufikia shule **24** mwaka **2016** ikiwa shule mbili zimeongezeka nazo ni;**Mzimuni, Mbezi juu na Mabwepande Tumaini Girls** shule ya kidato cha tano ya Wasichana.

CHANGAMOTO.

1. Upungufu wa walimu hasa katika masomo ya Sayansi na biashara.
2. Ufinyu wa maeneo ya ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa katika shule za mjini pamoja na viwanja vya michezo hasa kwa kata za **Tandale, Magomeni na Kinondoni**.
3. Upungufu wa miundombinu hasa madarasa,vyoo, nyumba za walimu na majengo ya utawala kwa shule zetu za sekondari.

MIKAKATI YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

1) Jitihada zinaendelea kufanyika ili kuuomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuajiri walimu wengi zaidi hasa wa masomo ya Sayansi na biashara.
2) Manispaa imeendelea kutenga fedha Kwa ajili ya fidia ilikuwapatia maeneo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na viwanja vya michezo kwa shule za Mjini. Jitihada zimeendelea kufanyika ili kuwashirikisha wadau na wahisani mbalimbali kusaidia ununuzi wa madawati kwa wanafunzi wa shule za Sekondari.
3) Halmashauri inatenga fedha ili kuwezakupunguza tatizo la miundombinu hasa madarasa, madawati, vyoo, nyumba za walimu n.k

SEKTA YA ELIMU MSINGI:

MAFANIKIO:

Hali ya Ufaulu kwa Wanafunzi wa darasa la saba kwa Mwaka **2015** inaonyesha jumla ya Wanafunzi **18,368** walifaulu mtihani wa Taifa kati ya wanafunzi **20,013** waliofanya mtihani. Pia wanafunzi **18,368** waliofaulu walichaguliwa kuendelea na Elimu ya Sekondari sawa na asilimia **100%.** Jumla ya Wanafunzi **14437** wa darasa la kwanza wameandikishwa kwa Mwaka **2016**, kati ya hao Wavulana ni **7229** na Wasichana ni **7208.** Aidha Mwaka **2016** jumla ya shule **236** zilifanya mtihani, kati yao wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza darasa la saba ni **20,013** waliofaulu ni **18,368** ambayo sawa na asilimia **91.8%.**

Changamoto

- Upungufu wa vyumba vya madarasa **1068**
- Upungufu wa vyoo vya wanafunzi wa kawaida **2751**
- Upungufu wa vyoo rafiki vya Walemavu **8**
- Upungufu wa nyumba za walimu **2110**
- Miundo mbinu iliyopo mingi inahitaji ukarabati.
- Shule **51** kati ya **78** za serikali hazina huduma ya maji Kwa kipindi chote cha mwaka.
- Shule **35** kati ya **78** za serikali hazina huduma ya umeme.
- Shule **48** kati ya **78** za serikali hazina huduma ya kompyuta

Mikakati ya kuondoa changamoto:

- Kushawishi wananchi kuchangia huduma za elimu.
- Halmashauri itumie vyanzo vya ndani kuboresha miundo mbinu ya shule.
- Serikali kuchangia ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu vyoo vya wanafunzi na ukarabati wa miundo mbinu chakavu.
- Kuhakikisha mazoezi ya kutosha ya mitihani yanatolewa mara kwa mara. Kwa mfano; mitihani ya wiki, mitihani ya Mock ya Kata, Wilaya na Mkoa.
- Kubaini idadi ya watoto wasiojua kusoma na kuandika katika kila shule hivyo kuanzisha mpango wa kuwasaidia.
- Kuhimiza utoaji wa chakula shuleni kwa wanafunzi hususani uji.

SEKTA YA BARABARA:

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ina jumla ya barabara zenye urefu wa kilometa **547.74**. Kati ya hizo barabara zenye urefu wa kilometa **72.15** zinamilikiwa na kuhudumiwa na TANROADS na

barabara zenye urefu wa kilometa **475.59** zinamilikiwa na kuhudumiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.Katika barabara zinazohudumiwa na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kilometa **134.4** ni za kiwango cha lami, kilometa **221.79** ni za kiwango cha changarawe na kilometa **119.4** ni za kiwango cha udongo.

CHANGAMOTO

1. Kuongezeka kwa wingi wa magari barabarani na hivyo kusababisha msongamano wa magari katika barabara kuu za Manispaa.
2. Uwezo mdogo wa Manispaa wa kujenga barabara zake kutoka kiwango cha changarawe na kuwa za lami.
3. Kuwa na bajeti ndogo ya matengenezo ya kawaida ya barabara za Manispaa kutoka mifuko mbalimbali ya fedha.
4. Ujenzi wa magorofa unaoendelea kwa kasi unaongeza uharibifu wa haraka kwa barabara mara zinapotengenezwa kwa kuwa zinapitisha uzito mkubwa wa vifaa vya ujenzi.
5. Ukosefu wa maabara ya manispaa inayotumika kupima ubora wa kazi za ujenzi wa barabara.

MIKAKATI

1. Manispaa itaendelea kutenga fedha za kujenga barabara kwa kiwango cha lami katika bajeti zake ili kuweza kuboresha urefu wa mtandao wa barabara na hatimaye kuweza kupunguza msongamano wa magari.
2. Kushawishi wananchi na sekta binafsi kuchangia ujenzi wa barabara za lami kwenye maeneo yao.
3. Kuendelea kushawishi **TAMISEMI** waongeze bajeti ya matengenezo ya barabara kupitia Mfuko wa Barabara.
4. Kushawishi TAMISEMI kutenga fedha maalumu kwa ajili ya ujenzi wa barabara za Lami katika Manispaa.

USAFISHAJI NA MAZINGIRA

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuboresha usafi wa mazingira kwa kuzingatia maeneo ya udhibiti wa taka ngumu, udhibiti wa maji taka, uelimishaji na uhamasishaji wa jamii ili iweze kushiriki vyema katika usafishaji mazingira yanayowazunguka, utafiti na uendelezaji wa teknolojia kutumia taka kama malighafi (Composting/Recycling/Reuse), upendezeshaji Manispaa (beautification).

MAFANIKIO

Katika mwaka **2015/16** Halmashauri imeimarisha usafi wa mazingira kwa kufanya mambo yafuatayo:-

- Kuimarisha kwa mfumo mpya wa udhibiti wa taka ngazi za mitaa
- Matangazo ya kuelimisha jamii juu ya usafi wa mazingira kwa kutumia njia mbalimbali kama vile vipeperushi, radio, TV, Loud speaker, vikao n.k.

- Ushirikishwaji wa wadau katika kutekeleza sheria ya uchafuzi wa mazingira kupitia adhabu ya papo kwa papo kwa kuwapa vikundi shirikishi vya usafi wa mazingira kwa kila Kata.
- Halmashauri imewashirikisha wadau mbalimbali wenye uwezo wa vifaa vya uzoaji taka ngazi ya mitaa.

Changamoto:

- Uwezo mdogo wa kudhibiti taka kulinganisha na kiasi kinachozalishwa.
- Ukosefu wa zana za kisasa za kutosha za kudhibiti taka.
- Umbali wa kufika dampo unaosababisha gharama kubwa ya mafuta ya magari ya taka.

MAPENDEKEZO YA MAKISIO NA MATUMIZI KATIKA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa;

Katika mwaka wa fedha **2017/2018** Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inatarajia kukusanya/kupokea fedha kiasi cha **Tsh. 160,832,112,680.00** Kati ya fedha hizo **Tsh. 105,350,084,680.00** ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu, **Tsh. 43,986,568,000.00** ni fedha za makusanyo ya ndani ya Halmashauri, **Tsh. 979,800,000.00** za michango ya nguvu za wananchi na kiasi cha **Tsh.10,515,660,000.00** ni kutoka TAMISEMI kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa barabara (Road Fund).

JEDWALI 1: MUHTASARI WA BAJETI KWA MWAKA 2017/2018

RUZUKU ZA SERIKALI	MCHANGO WA WANANCHI	MAPATOYA NDANI	MFUKO WA BARABARA	JUMLA
105,350,084,680.	979,800,000.	43,986,568,000.	10,515,660,000.	160,832,112,680
65%	1%	27%	7%	100%

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa;

Kiasi cha **Tsh. 105,350,084,680.00** za ruzuku kutoka Serikali Kuu kinajumuisha kiasi cha **Tsh.53,890,399,600.00** ikiwa ni mishahara, kiasi cha **Tsh. 4,325,946,608.00** ni matumizi ya kawaida na kiasi cha **Tsh.47,133,738,472.00** fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo toka Serikali Kuu.Aidha, Halmashauri inatarajia kupokea kiasi cha **Tsh.10,515,660,000.00** ambayo ni ruzuku kutoka mfuko wa matengenezo ya barabara - TAMISEMI (Road Fund).

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa;

Mpango huu umelenga katika kufikia dhima na dira ya Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kwa kutekeleza malengo yafuatayo: -

A) Huduma ya ukimwi kuboreshwa na maambukizi mapya kupunguzwa
B) Uboreshaji, uendelezaji na utekelezaji kikamilifu mpango wa Taifa wa kupambana na rushwa.
C) Kuimarika kwa upatikanaji na ubora wa huduma za jamii
D) Kuongezeka na kuboreka kwa huduma za kiuchumi na miundombinu
E) Kuimarika kwa utawala bora na utoaji wa huduma
F) Kuimarika kwa uwezo wa kiuchumi na kijinsia na ustawi wa jamii
G) Kuimarika kwa usimamizi wa kujikinga na maafa na milipuko ya magonjwa

H) Kuimarika kwa usimamizi wa maliasili na mazingira

MAKISIO YA MATUMIZI KWA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

Katika mwaka wa fedha **2017/2018** Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inatarajia kutumia fedha kiasi cha **Tsh. 160,832,112,680.00** Kati ya fedha hizo **Tsh. 70,121,041,070.00** ni matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na asilimia **44** ya bajeti yote na **Tsh.90,711,071,610.00** ni fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ni sawa na asilimia **56** ya bajeti. Angalia jedwali namba 3 na 4, 5 na 6

JEDWALI NA. 3: MAKISIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2017/2018

MISHAHARA	MATUMIZI YA KAWAIDA (PE &OC)	MIRADI YA MAENDELEO	JUMLA
VYANZO VYA NDANI	**11,904,694,862.00**	32,081,873,138.00	43,986,568,000.00
RUZUKU YA SERIKALI KUU	**58,216,346,208.00**	**47,133,738,472.00**	**105,350,084,680.00**
MFUKO WA BARABARA	0	**10,515,660,000.00**	**10,515,660,000.00**
MICHANGO YA WANANCHI	0	979,800,000.00	979,800,000.00
JUMLA	**70,121,041,070.00**	**90,711,071,610.00**	**160,832,112,680.0**
ASILIMIA	**44%**	**56%**	**100%**

JEDWALI NA.4: MAKISIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA

MGAWANYO	VYANZO VYA NDANI	RUZUKU YA SERIKALI KUU	JUMLA
MISHAHARA	1,330,450,000.00	**53,890,399,600.00**	55,220,849,600.00
MATUMIZI YA KAWAIDA	10,574,244,862.00	**4,325,946,608.00**	14,900,191,470.00
JUMLA	**11,904,694,862.00**	**58,216,346,208.00**	**70,121,041,070.00**
ASILIMIA	**17%**	**83%**	**100%**

JEDWALI NA.5: MAKISIO YA MATUMIZI YA MIRADI YA MAENDELEO MWAKA 2017/2018

VYANZO VYA NDANI	MCHANGO WA WANANCHI	TFDA, NHIF, COST SHIRING	RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU	MFUKO WA BARABARA	JUMLA
27,780,001,138.00	979,800,000.00	4,301,872,000.00	47,133,738,472.00	**10,515,660,000.00**	**90,711,071,610.00**
31%	**1%**	**5%**	**52%**	**11%**	**100%**

JEDWALI NA.6: MCHANGANUO WA MATUMIZI YA MAPATO YA NDANI BAJETI YA MWAKA 2017/2018

CHANZO CHA FEDHA	MIRADI YA MAENDELEO	TFDA, NHIF, COST SHIRING	MATUMIZI YA KAWAIDA	MISHAHARA	JUMLA
VYANZO VYA NDANI	27,780,001,138.00	4,301,872,000.00	10,574,244,862.00	1,330,450,000.00	**43,986,568,000.00**
ASILIMIA	**63%**	**10%**	**24%**	**3%**	**100%**

Aidha Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imetimiza vigezo vya kutenga asilimia **60** ya mapato ya ndani kutumika katika miradi ya maendeleo. Hivyo jumla ya **Tsh. 27,780,001,138.00** sawa na asilimia **63** ya bajeti ya makusanyo ya ndani imetengwa kwaajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

NGUVU ZA WANANCHI:

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa, Wananchi wanatarajiwa kuchangia nguvu na fedha taslimu zenye jumla ya thamani ya **Sh. 979,800,000.00** katika miradi yote itakayotekelezwa mwaka **2017/2018**. Kiasi hiki kimo ndani ya Bajeti yetu ya mapato ya ndani.

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa, Ili kutumia fedha za Serikali kwa kuzingatia miongozo, nachukua nafasi hii kuwaeleza kuwa fedha za Ruzuku ya maendeleo zinaletwa pamoja na miongozo ya matumizi yake, ni vyema tukajikita zaidi katika kukusanya fedha zetu za ndani (own source), ili kuwa na uhakika wa kuweza kuendesha Halmashauri yetu pamoja na kutekeleza miradi ya maendeleo.

UMBILE LA BAJETI 2017/2018:

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa, baada ya maelezo haya sura ya bajeti ya mwaka 2017/2018 inakuwa kama ifuatavyo:

UMBILE LA BAJETI YA MWAKA 2017/2018

MAPATO/MATUMIZI	MAPATO HALISI 2015/16	BAJETI YA MWAKA 2016/17	MAKISIO YA BAJETI 2017/18	MAOTEO KWA MWAKA 2018/19	MAOTEO KWA MWAKA 2019/20
A: MAPATO					
JUMLA YA MAKUSANYO KWA VYANZO VYA NDANI	48,371,744,826.05	38,571,414,000.00	**43,986,568,000.00**	51,010,695,015.00	67,461,644,157.34
Mchangowawananchi	1,356,390,720.00	852,000,000.00	979,800,000.00	1,126,770,000.00	1,490,153,325.00
JUMLA YA MAKUSANYO YA HALMASHAURI	**49,728,135,546.05**	**39,423,414,000.00**	**44,966,368,000.00**	**52,137,465,015.00**	**68,951,797,482.34**
MAPOKEZI YA FEDHA KWA MATUMIZI YA KAWAIDA - RUZUKU				0.00	0.00
(i) Mishahara PE	94,102,077,012.92	48,663,241,400.00	53,890,399,600.00	77,228,564,101.80	102,134,776,024.63
(ii) Matumiziyakawaida - OC	1,925,275,504.04	2,819,354,304.00	4,325,946,608.00	4,536,733,888.50	5,999,830,567.54
JUMLA NDOGO	**96,027,352,516.96**	**51,482,595,704.00**	**58,216,346,208.00**	**81,765,297,990.30**	**108,134,606,592.17**
MAPOKEZI YA FEDHA KWA MIRADI YA MAENDELEO - RUZUKU			-	0.00	0.00
LGDG - FOREIGN (CDG)		0	0.00	0.00	0.00
LGDG - RUZUKU YA SERIKALI - KUJENGA UWEZO		0	308,259,208.00	0.00	0.00
LDGD - RUZUKU YA SERIKALI FEDHA ZA NDANI	-	3,082,592,084.00	2,774,332,876.00	4,076,728,031.09	4,688,237,235.75
MAJI VIJIJINI - FEDHA ZA NDANI	-	0	0.00	0.00	0.00
MAJI VIJIJINI - FEDHA ZA NJE	-	60,670,000.00	55,280,000.00	80,236,075.00	92,271,486.25
KAMPENI YA KITAIFA YA USAFI - MAJI	-	0	0.00	0.00	0.00
ROAD FUND - MAENDELEO - RUZUKU TOKA TAMISEMI	8,246,730,512.01	8,048,243,867.00	10,515,660,000.00	10,643,802,514.11	12,240,372,891.22
HIV - MRADI WA KUTOKOMEZA UKIMWI	-	0	0.00	0.00	0.00
LDF - RUZUKU YA KUENDELEZA MIFUGO		4,932,500.00	4,932,500.00	6,523,231.25	7,501,715.94
DADPS BASIC - (A-CBG) - KILIMO KUJENGA UWEZO		0	0.00	0.00	0.00
DADPS- (A-EBG) KILIMO - MAENDELEO		0	0.00	0.00	0.00
DMDP		**51,126,222,000.00**	**41,907,650,998.00**	**67,614,428,595.00**	**77,756,592,884.25**
MMEM - MPANGO MAALUMU WA ELIMU YA MSINGI		0	0.00	0.00	0.00
MMES -MPANGO MAALUMU WA ELIMU YA SEKONDARI	-	0	60,670,000.00	0.00	0.00
HBF - MFUKO WA KUCHANGIA AFYA - WAFADHILI	2,012,223,000.00	1,830,940,890.00	1,830,940,890.00	2,421,419,327.03	2,784,632,226.08
MFUKO WA JIMBO	176,522,000.00	88,261,000.00	118,072,000.00	116,725,172.50	134,233,948.38
MMAM - MFUKO MAALUMU WA AFYA YA	-	0	0.00	0.00	0.00

MAPATO/MATUMIZI	MAPATO HALISI 2015/16	BAJETI YA MWAKA 2016/17	MAKISIO YA BAJETI 2017/18	MAOTEO KWA MWAKA 2018/19	MAOTEO KWA MWAKA 2019/20
MSINGI					
MAJI VIJIJINI		55,280,000.00	0	73,107,800.00	84,073,970.00
TASAF		0	0.00	0.00	0.00
SHULE MAALUMU		73,600,000.00	73,600,000.00	97,336,000.00	111,936,400.00
JUMLA NDOGO	**10,435,475,512.01**	**64,370,742,341.00**	**57,649,398,472.00**	**85,130,306,745.97**	**97,899,852,757.87**
JUMLA YA FEDHA ZA SERIKALI KUU MIRADI NA MATUMIZI YA KAWAIDA	**106,462,828,028.97**	**115,853,338,045.00**	**115,865,744,680.00**	**153,216,039,564.51**	**176,198,445,499.19**
JUMLA YA MAPATO YA HALMASHAURI	**156,190,963,575.02**	**154,248,195,864.00**	**160,832,112,680.00**	**203,993,239,030.14**	**234,592,224,884.66**
B: MATUMIZI	**-**		-	0.00	0.00
MATUMIZI YA KAWAIDA KWA FEDHA ZA NDANI			-	0.00	0.00
(i) Mishahara PE	707,291,120.68	1,027,080,000.00	1,330,450,000.00	1,358,313,300.00	1,562,060,295.00
(ii) Matumiziyakawaida	5,932,051,774.42	4,786,192,270.47	10,574,244,862.00	6,329,739,277.70	7,279,200,169.35
(iii) Ada yasekondari	63,632,600.00	0	0.00	0.00	0.00
(iv) UchangiajiHudumazaAfya	4,477,151,706.85	3,215,280,000.00	3,774,712,000.00	4,252,207,800.00	4,890,038,970.00
(v)National insurance health fund - NHIF		432,000,000.00	496,800,000.00	571,320,000.00	657,018,000.00
(vi)Tanzania Food and Drugs Authority - TFDA		26,400,000.00	30,360,000.00	34,914,000.00	40,151,100.00
JUMLA YA FEDHA ZA NDANI KWA MATUMIZI YA KAWAIDA	**11,180,127,201.95**	**10,571,611,094.00**	**16,206,566,862.00**	**13,980,955,671.82**	**16,078,099,022.59**
FEDHA ZA RUZUKU KWA MATUMIZI YA KAWAIDA			0.00	0.00	0.00
(i) Mishahara PE	94,102,077,012.92	48,663,241,400.00	53,890,399,600.00	64,357,136,751.50	74,010,707,264.23
(ii) Matumiziyakawaida	1,925,275,504.04	2,819,354,304.00	4,325,946,608.00	3,728,596,067.04	4,287,885,477.10
JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA FEDHA ZA RUZUKU	**96,027,352,516.96**	**51,482,595,704.00**	**58,216,346,208.00**	**68,085,732,818.54**	**78,298,592,741.32**
C: MATUMIZI YA FEDHA ZA MIRADI KWA FEDHA ZA NDANI			-	0.00	0.00
MATUMIZI KWENYE MIRADI	13,618,678,183.77	27,113,247,725.00	27,780,001,138.00	35,857,270,116.31	41,235,860,633.76
NGUVU ZA WANANCHI	1,356,390,720.00	710,000,000.00	979,800,000.00	938,975,000.00	1,079,821,250.00
JUMLA NDOGO	**14,975,068,903.77**	**27,823,247,725.00**	**28,759,801,138.00**	**36,796,245,116.31**	**42,315,681,883.76**
D: MATUMIZI YA MIRADI KWA FEDHA ZA RUZUKU			-	0.00	0.00
RUZUKU TOKA SERIKALI KUU-(GOVERNMENT GRANTS)	1,465,642,011.96	5,196,275,474.00	3,082,592,084.00	6,872,074,314.37	7,902,885,461.52
WADAU - (DEVELOPMENT PARTNERS)		51,126,222,000.00	44,051,146,388.00	67,614,428,595.00	77,756,592,884.25
MFUKO WA BARABARA	**7,614,974,801.52**	8,048,243,867.00	10,515,660,000.00	10,643,802,514.11	12,240,372,891.22
JUMLA YADHA ZA RUZUKU-MIRADI	**24,055,685,717.25**	**64,370,741,341.00**	**57,649,398,472.00**	**85,130,305,423.47**	**97,899,851,236.99**
JUMLA YA MATUMIZI YA HALMASHAURI	**131,263,165,436.16**	**154,248,195,864.00**	**160,832,112,680.00**	**203,993,239,030.14**	**234,592,224,884.66**

MWISHO:

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe Waalikwa; Halmashauri imejipanga kutekeleza Maelekezo ya Serikali ya awamu ya tano ambayo inasisitiza kuwa uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kuongeza ajira kwa vijana ili kupunguza umaskini hasa wa kipato, kuimarisha utawala bora na kuthibiti matumizi ya serikali yasiyokuwa ya lazima. Bajeti ya mwaka **2017/2018** ni mwendelezo wa Halmashauri kutekeleza Malengo ya Millenia na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Ili kufikia malengo tuliyojiwekea hatuna budi kuhakikisha kila mwananchi anashiriki kikamilifu katika kutumia fursa zilizopo katika kuleta maendeleo na kuondokana na umaskini.

Ni vizuri ikaeleweka kwamba Halmashauri ni chombo cha wananchi ambacho kimewekwa kisheria kushirikiana na wananchi katika uzalishaji ili kuongeza ajira na kujiletea maisha bora.

Waheshimiwa Madiwani na Wajumbe waalikwa, baada ya kusema hayo naomba sasa kutoa hoja.

Benjamini Kawe Sitta
MSTAHIKI MEYA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI